# FASIHI YA KISWAHILI: MUSTAKABALI WA TANZANIA KATIKA MUKTADHA WA UTANDAWAZI

*Gerephace Mwangosi* na *Mussa E. Msamilah*

**Ikisiri**

*Wanazuoni wengi wa ndani na nje ya Afrika wanatumia mbinu mbalimbali za kisanaa ili kueleza masuala yanayosawiri hali halisi iliyopo katika mataifa yao. Baadhi ya masuala yanayoelezwa ni pamoja na kutamalaki kwa utandawazi na athari zake katika mataifa yanayoendelea. Makala hii imeeleza nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika kuimarika kwa utandawazi katika nchi za Kiafrika kwa kipindi cha miongo mitatu iliyopita. Katika kipindi hiki, mataifa ya Kiafrika yameshuhudia mapinduzi makubwa katika mifumo ya siasa na sera za uchumi huria unaodhibitiwa na mataifa ya kibepari. Kwa hiyo, makala hii imechunguza athari za utandawazi nchini Tanzania kwa kurejelea riwaya teule za Bina-Adamu (2002) ya K. W. Wamitila na Msomi Aliyebinafsishwa (2012) ya N. Nyangwine. Riwaya hizi zimeteuliwa kwa kuwa zinaakisi vizuri hali halisi ya harakati na athari za utandawazi hapa nchini. Pia, inadokeza mustakabali wa Tanzania ya sasa na ijayo. Data za makala hii zilipatikana maktabani. Nadharia ya Uhalisia imetumika katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa. Makala inahitimisha kuwa kadiri harakati za utandawazi zinavyozidi kuimarika nchini, ndivyo mifumo ya kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi inavyozidi kudhoofika na kuporomoka.*

## Utangulizi

Riwaya ya Kiswahili katika muktadha wa Tanzania na kwingineko barani Afrika ni miongoni mwa vyombo nyeti vinavyohakiki hali na athari za utandawazi kwa takribani miongo mitatu sasa. Makala hii ni zao la uchunguzi uliofanywa kuhusu athari za utandawazi nchini Tanzania kwa kurejelea riwaya za *Bina-Adamu* (2002) na *Msomi Aliyebinafsishwa* (2012). Riwaya hizi ni matokeo ya mabadiliko makubwa katika sekta za utawala na uchumi yaliyofanyika mwanzoni mwa miaka ya 1990 baada ya kuanzishwa na kuimarika kwa sera za utandawazi hapa nchini (Bhalla, 2006).

Utandawazi ni dhana inayotumiwa kuelezea mikabala ya kiutamaduni, kielimu, kiuchumi na hata kisiasa inayosisitiza maungano na mahusiano yanayovuka mipaka ya taifa moja na lingine. Utandawazi una dhamira ya kuondoa vikwazo vyote vya kijiografia na kisiasa ili kuruhusu mtiririko huru wa nguvu kazi, itikadi, lugha na teknolojia baina ya mataifa ya ulimwengu (Sullivan, 1994). Aidha, utandawazi unaeleza mfungamano na uhusiano uliojitokeza katika miaka 30 iliyopita, hasa katika biashara na uchumi duniani. Mfungamano na uhusiano huo umepata kasi

kubwa ya kuweka mitaji na kunufaika kiuchumi na kiutamaduni; ukisaidiwa na maendeleo makubwa ya teknolojia ya mawasiliano yaliyoondoa vikwazo vya masafa na wakati.

Kihistoria, utandawazi hauwezi kuepushwa na misingi ya mikakati ya G7, Benki ya Dunia, IMF na WTO, vyombo vya kibepari vinavyosimamia, kuimarisha na kuendeleza itikadi ya uliberali mpya (Jauch, 2001). Kinadharia, mfungamano wa utandawazi katika jamii za kimataifa unatazamwa kwa namna mbili. Kambi ya kwanza huutazama utandawazi kuwa ni baraka na una faida kubwa, hasa kwa nchi zinazoendelea kwa kuwa huboresha maisha, hufungua milango ya biashara, masoko huria ya bidhaa na kuufanya utamaduni wa taifa moja ukutane na ule wa mataifa mengine (Offiong, 2001).

Kambi ya pili, kwa kutumia ithibati jarabati, inakanusha uhalali wa madai ya kambi ya kwanza, kwamba, utandawazi si dhana mpya, bali ni upeo wa dhana kongwe yenye sifa mpya ya kutumia maendeleo makubwa yaliyopatikana kiteknolojia na kunyonya utajiri wa dunia. Kwa sehemu kubwa, mabadiliko yaliyotokea mwanzoni mwa miaka ya 1970 yalisababishwa na maslahi ya kibiashara na utashi wa mataifa makubwa yaliyolenga kupata faida kubwa kupita kiasi (Nicol, 2002). Huu ndio msingi wa makala hii kuchunguza athari za utandawazi katika muktadha wa Tanzania kwa kurejelea riwaya teule.

Licha ya kuwa riwaya ya Kiswahili imekuwa ikichunguza masuala ya kijamii kwa namna mbalimbali, bado wahakiki wengi wamejikita zaidi katika uhakiki wa vipengele vya maudhui na fani yake. Ili kupanua mawanda ya kuihakiki, kuna haja ya kutilia mkazo uhusiano uliopo kati ya riwaya na taaluma nyingine. Kwa kufanya hivyo, utanzu huu utakua na kukomaa kupitia uhakiki wake katika mikabala ya taaluma nyingine. Katika jitihada za kulifanya jambo hili kwa vitendo, makala hii imechunguza athari za utandawazi katika jamii za Tanzania kwa kurejelea riwaya teule za *Bina–Adamu* (2002) na *Msomi Aliyebinafsishwa* (2012). Mkazo ulizingatia kuwa riwaya ya Kiswahili ni mojawapo ya nyenzo imara inayohakiki kuimarika kwa utandawazi katika jamii za Kiafrika.

**Mustakabali wa Tanzania katika Muktadha wa Utandawazi**

Katika karne ya 21, bara la Afrika limepitia mabadiliko makubwa, hasa katika sekta za kisiasa na kiuchumi kutokana na kuingia kwa mfumo wa utandawazi. Licha ya kuwa utandawazi umekuwapo kwa muda mrefu katika mataifa ya Kimagharibi, Afrika imekumbatia dhana hii kwa ukamilifu wake mwishoni mwa karne ya 20 na mwanzo mwa karne ya 21 (Sullivan, 1994). Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba utandawazi haukuwapo hapo kabla. Utandawazi ulikuwapo, isipokuwa mkabala wa Kimagharibi ndio umefyaziwa kwayo na kutenga ule wa Kiafrika (Kamau, 2005).

Kwa hiyo, utandawazi barani Afrika unaweza kubainishwa katika sura mbalimbali kutegemeana na wakati unaolengwa.

Utandawazi katika mtazamo wa Kiafrika ulikuwa kama falsafa ya maisha iliyoongoza namna ya kuhusiana na wenzao, Mungu na hata mazingira yaliyowazunguka (Little, 1996). Kwa namna hali ilivyo sasa, utandawazi umesababisha maingiliano ya hali ya juu ya mataifa ya ulimwenguni; na kuleta mtagusano na ukuruba kati ya mataifa yaliyoendelea na yale yanayoendelea (Amatubi, 2002). Mwonoulimwengu wa waandishi kuhusu falsafa ya utandawazi ni jambo linaloelekea kudhihirika vyema katika riwaya za Kiswahili. Riwaya zilizorejelewa katika makala hii zinalenga kudhihirisha athari za utandawazi nchini Tanzania kama zilivyobainishwa katika sehemu inayofuata.

**Kudhoofika kwa Uchumi na Misingi Yake**

Athari mojawapo ya utandawazi nchini Tanzania ni kudhoofika kwa uchumi na misingi yake. Kudhoofika huko ni zao la uwekezaji wa mabepari kutoka katika nchi za ughaibuni. Uwekezaji ni hali ya kutumia fedha au mali katika biashara kwa lengo la kuzalisha zaidi (TUKI, 2004). Ubepari hutumia njia mahususi kufanikisha madhumuni yao kama vile kutoa misaada na mikopo kwa nchi zinazoendelea yenye masharti nafuu, riba kubwa na matumizi ya sera za soko huria, zikiwamo taasisi za kifedha kama Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Dunia (Little, 1996). Mfumo huu mara nyingi hushindwa kujitosheleza kwa mahitaji yake ya ndani ya nchi inayohusika. Hivyo, hulazimika kutoka nje ya mipaka yake ili kukidhi mahitaji kwa mbinu za uwekezaji.

Katika miaka ya hivi karibuni, nchi za Kiafrika zimekuwa na sera na sheria za kulinda uwekezaji. Hali hii ni matokeo ya mataifa ya kipebari kutumia mbinu za hali ya juu kuhakikisha maslahi yao yanatimizwa. Uwekezaji ni miongoni mwa mbinu za ukoloni mamboleo ambao una uwezo wa kujidhihirisha katika hali mbalimbali kama vile kutoa misaada kwa Waafrika (Mbonde, 2005). Misaada hiyo huambatana na masharti magumu ya utekelezaji wa mikopo watoayo. Hali hii huyafanya mataifa ya kibepari kunyakua kila sekta ya kiuchumi katika nchi zinazoendelea kwa rahisi na gharama nafuu.

Hali ya kufutwa kwa mipaka ya kimataifa husababisha wananchi katika nchi za ulimwengu wa tatu, ikiwamo Tanzania, kukosa fursa zilizokuwa zimejengwa katika misingi imara ya vitega-uchumi vya taifa. Vilevile, miradi yake kama vile viwanda, kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara huendelea kuzorota kwa kasi (Timammy, 1990). Mwandishi anadhihirisha jambo hili kupitia sauti ya waandamanaji:

Viwanda vimeuliwa! Tumeletewa bidhaa chapwa! Watatulisha sumu hawa! Lakini upande wa serikali walikuwa wanasema haya ndiyo maendeleo, hatuwezi

> kuyakwepa. Ulimwengu sasa ni kijiji. Hii ndiyo maana ya *Free Market Economy and Liberisation*! ... Hapana haja ya kupitia hatua zote za ukuaji, tunaweza kuruka nyingine ili twende sambamba na wakati (Wamitila, 2002: 51).

Nukuu hii inaonesha jinsi nchi za dunia ya tatu zinavyotazamwa kama dampo la bidhaa zisizofaa katika mataifa ya dunia ya kwanza. Pia, inaonesha zinavyoandamwa na utegemezi wa misaada na mikopo kutoka nchi tajiri ili kukidhi mahitaji ya bajeti zao. Jambo la kusikitisha ni kwamba, rasilimali zilizopo hazitumiki ipasavyo kiasi kwamba nchi changa zinanunua hata vitu zinavyoweza kuzalisha. Nchi za kibepari hufanya jitihada kubwa za kukwamisha na kuzuia misaada ya kiuchumi ili kutekeleza mahitaji yao. Mwandishi anasema:

> Wanayo lakini idhini ya kuwavua, sisi tunayo. Wapatikana kwenye maji ya kimataifa, *International Waters* … wanapenda sana hawa wa makopo? Kwao ndio maendeleo hayo! Wakiyagomea, nasi misaada ya kiuchumi kwao tunaizuia! (Wamitila, 2002: 50).

Haya ni baadhi ya madhara ya misaada ya nchi tajiri kwa mataifa yanayoendelea. Pia, inaonesha namna wazawa wanavyopenda vyakula vya makopo na jinsi wanavyobanwa kwa masharti magumu. Kuna haja ya nchi zinazoendelea kuchukua hatua madhubuti za kujikwamua kiuchumi ili kuepuka utegemezi. Viongozi hawana budi kufanya tathmini ya kina kuhusu faida na hasara za utandawazi hapa nchini, kisha hatua muafaka zichukuliwe kuukabili kwa vitendo.

**Dhuluma na Uporaji wa Rasilimali**

Uwekezaji ni mojawapo ya matokeo ya ubeberu ambao ni ubepari uliokomaa na kuvuka mipaka ya nchi yake na kuingia nchi nyingine kwa madhumuni ya kunyonya uchumi wa nchi inayohusika. Jitihada za ubepari kunyonya uchumi katika mataifa yanayoendelea unaambatana na dhuluma na uporaji wa rasilimali za umma na wananchi. Mahali pengine, wananchi wametumbukizwa katika hali ngumu ya maisha na umaskini wa kutupwa na kuwa watumwa katika nchi yao (Mayega, 2006). Jambo la kusikitisha ni kwamba, hata wananchi wakitoa mapendekezo kuhusu namna sahihi ya kunufaika na rasilimali zilizopo katika maeneo wanayoishi hupuuzwa na kutosikilizwa. Mwandishi anathibitisha hali hiyo kupitia kwa Nyagichuro:

> Hili ndilo bonde lililonifikisha hapa nilipo. Kabla ya kulibinafsisha lilisaidia kunisomesha kwa hao walalamishi kujilimia mazao na kuvuna samaki. Baada ya kulibinafsisha siku hizi bado naendelea kufaidi ile teni pasenti kutoka kwa Mzungu! Hakika hao walalamishi wataendelea kulalamika lakini mimi nitaendelea kula teni pasenti kwa kipindi chote cha uwekezaji (Nyangwine, 2012: 57-58).

Nyagichuro akiwa madarakani aliamua kulibinafsisha bonde la Remerera lililokuwa tegemeo pekee kwa uchumi na ustawi wa Wanakong'amu waliomlea na kumsomesha. Matokeo yake, Wanakong'amu waliangukia katika mateso na kutumbukia katika umaskini mkubwa. Wito wa makala hii unazitaka serikali za nchi za dunia ya tatu zilitazame jambo hili kwa maslahi mapana ya uchumi na maendeleo ya wananchi wao. Uwekezaji umejaa ulaghai na dhuluma hasa ukichunguza namna unavyofanyika katika nchi za dunia ya tatu kama vile Tanzania.

**Uharibifu wa Mazingira na Athari Zake**

Katika miaka ya hivi karibuni nchi nyingi barani Afrika zimekuwa na sera na sheria za kulinda wawekezaji katika miradi mbalimbali. Licha ya kufanya hivyo, hakuna uwiano mzuri wa kimaslahi na kiuchumi ili kunufaika kikamilifu katika miradi iliyowekezwa (Hussein, 1971). Mahali pengine, nchi za Kiafrika hazifaidi chochote zaidi ya kuachiwa mashimo kwa upande wa sehemu zenye machimbo ya madini, sumu kwenye vyanzo vya maji, uchafuzi na uharibifu mkubwa wa mazingira, kuharibiwa kwa makazi ya wananchi bila kupewa fidia, pamoja na maangamizi ya uoto wa asili (Krantz, 2001; Mwalongo, 2015). Wananchi wamekuwa wakishuhudia namna rasilimali katika taifa lao zinavyoporwa na mazingira kuharibiwa kwa kasi bila kuchukua hatua zinazolenga kuyanusuru. Wamitila (2002:28) anaeleza:

> Yale mashimo uliyoyaona yalikuwa na madini: shaba, dhahabu, fedha na ulanga ... walihimizwa kuyachimba kwa ahadi ya kulipwa lakini mpaka leo hawana walichokiona! Waliofaidi ni wale waliowapora madini haya. Kituo cha pili tulichokwenda kilikuwa na mashimo makubwa labda ya madini. Hapakuwa na mmea hata mmoja.

Mwandishi katika nukuu hii anaonesha athari za uwekezaji kwa upande wa mazingira. Hali hii inaonesha namna uwekezaji usivyo na tija kwa mazingira, uchumi na maendeleo ya taifa na wananchi. Mathalani, miradi ya makampuni makubwa ya uchimbaji wa madini kama vile Geita Gold Main Company na North Mara Main Company huleta athari kubwa kwa upande wa mazingira, ukiwamo uchafuzi wa vyanzo vya maji na uharibifu wa uoto wa asili. Katika maeneo ya miradi hiyo, jamii imetumbukia katika migogoro mikubwa baina ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Jambo hilo linasababisha misukosuko kwa raia kutokana na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na maendeleo yake.

Sera na sheria za kuwalinda na kuwatengenezea mazingira rafiki wawekezaji ni suala linalofanywa na baadhi ya viongozi bila uzalendo unaojali maslahi mapana ya taifa na wananchi wake. Mikakati hiyo haiendi sambamba na kuweka kanuni za namna ya kuwanufaisha wananchi katika maeneo yanayohusika na uwekezaji. Matokeo yake, wananchi huachiwa athari zilizotajwa hapo juu. Hali hiyo

iliwafanya Wanakong'amu katika riwaya ya *Msomi Aliyebinafsishwa* kulazimika kumwandikia barua Nyagichuro. Barua inaeleza:

> Nyagichuro, umekubali ardhi ya mizimu ya babu zetu iwekwe mikononi mwa watu weupe! Na zawadi uliyopata ni kwenda kusoma Ulaya na wawekezaji! Umekubali kila kitu kiwekezwe hapa kijijini, hata nyumba za viongozi wetu! Wananchi wa Kong'amu tunauawa na Wazungu kwa kupigania bonde la Remerera. Hatuna ardhi, yenye rutuba imekwishanyakuliwa. Bonde ulililoliuza wewe kwa Mzungu! Kumbuka bonde la Remerera ndilo lililokukuza hadi hapo ulipo! (Nyangwine, 2012: 55-56).

Mwandishi anamtumia Nyagichuro kueleza ukweli wa maisha ya Waafrika walio wengi kuhusu madhara wanayopata katika baadhi ya sehemu ambako taratibu za uwekezaji hazikufuatwa na kuzingatiwa. Hali hiyo husababisha wananchi wengi kukosa imani na serikali yao kwa upande wa usimamizi wa rasilimali zilizopo nchini pamoja na maslahi yake (Mwalongo, 2015). Hapana shaka kuwa uwekezaji umejaa ulaghai na dhuluma, hasa ikichunguzwa namna unavyofanyika nchini Tanzania.

Licha ya Wanakong'amu kutaka mabadiliko yafanyike ili kurekebisha sera za uwekezaji na ubinafsishaji katika jamii yao, isivyo bahati, viongozi wao waliwabeza na kuwapuuza; badala yake, walisisitiza somo la ubinafsishaji lifundishwe kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Uwekezaji umejenga mianya ya kupandikiza viongozi katika nchi zinazoendelea ili kupata fursa pana katika jitihada na harakati zao za uwekezaji (Kivutha, 1999). Mzee Gonto Goyoka alichangiwa na wawekezaji fedha za kigeni ili kuwahonga wapiga kura. Hali hiyo ilimfanya kupiga marufuku nyimbo zote zilizopinga uwekezaji na ubinafsishaji katika jamii ya Kong'amu. Kiongozi huyu hakuzingatia kuwa fasihi ni chombo cha kuelezea matamanio ya jamii (Sengo, 1973).

**Ugumu wa Kuvunja Sura za Ubepari**

Wandishi wameonesha jinsi mataifa ya kipebari yanavyotumia mbinu za hali ya juu kuhakikisha maslahi yao yanatimizwa. Ukoloni mamboleo unajidhihirisha katika sura mbalimbali, na ni vigumu kudhibitiwa. Baadhi ya mawakala wake ni Huntha mwenye jinsi zote mbili, akimaanisha ubeberu na ukoloni mamboleo. Hali ya kuwa na jinsi zote mbili inamaanisha ugumu wa kuudhibiti ukoloni mamboleo katika nchi za dunia ya tatu. Mwingine ni PP (Peter Pan) ambaye ni mmoja wa viongozi maarufu wa propaganda duniani aliyetokea Marekani na anaiwakilisha nchi ya Marekani kwa propaganda zinazotawala dunia nzima ili kuyaneemesha mataifa tajiri.

Zipo jitihada za itikadi za kibeberu zinazolenga kuziangamiza juhudi za Umoja wa Afrika zenye madhumuni ya kujikomboa katika nyanja zote za kijamii. Tangu uhuru upatikane katika nchi za Kiafrika kumekuwa na juhudi za kujikomboa kisiasa, kiuchumi, kielimu na kiutamaduni kwa kuunda jumuiya za kikanda kama vile Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Afrika Magharibi, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika, pamoja na Umoja wa Mataifa ya Afrika. Hata hivyo, jitihada zinazofanyika zinadhoofishwa na mataifa ya kibeberu kwa kuwa nchi nyingi za Afrika zimebaki na uhuru wa bendera tu.

Matokeo ya juhudi za kuzuia Umoja wa Afrika yalishuhudiwa pale Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipovunjika rasmi miaka kumi tu baada ya kuundwa mwaka 1967 (Ryanga, 2003). Nchi wanachama zilibaki zikilaumiana kuhusu chanzo cha kuvunjika kwa jumuiya. Baadhi ya nchi zililaumiwa kwa kuhimizwa na mataifa ya kibepari ili kuivunja jumuiya. Hali hiyo ilizirahisishia nchi za kibeberu kunufaika, hasa kwa upande wa soko la ndani la nchi hizo.

**Kuporomoka kwa Uzalendo na Uwajibikaji**

Viongozi wamechorwa katika sura tofauti tofauti zinazohalisika kulingana na namna wanavyojipambanua kwa kuwa wengi wao wamejaa ubadhilifu, usaliti, rushwa, ubinafsi, uchoyo, uchu wa madaraka na kutaka kutawala daima. Viongozi hao hawafanyi tathmini kuhusu ubora na udhaifu wao katika kusimamia utekelezaji wa mipango na sera za maendeleo ya mataifa wanayoyaongoza (Murray, 2000; Mpangala, 2007). Wengi wao hujilimbikizia mali na kuwasababishia wananchi hali ya umaskini uliokithiri.

Suala la uongozi mbaya limekuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Taifa lolote likiathirika na kadhia hii ni vigumu kujijengea uwezo wa kutoa huduma nzuri kwa wananchi wake. Mwandishi amemtumia mhusika X anayesimama badala ya viongozi wa mataifa yanayoendelea wanaouza utu wao na kubeza asili yao kwa kuvaa Uzungu. Viongozi hao hutumika kunyonya rasilimali za mataifa yao kwa mgongo wa utaalamu. Baadhi ya wabunge wanaubariki na kuupokea uwekezaji bila kuchunguza na kupima uwiano uliopo kati ya faida na hasara zake kwa kuzingatia maslahi mapana ya taifa na maendeleo yake. Mwandishi anaeleza:

> Wabunge wetu wanaona! Wanaubariki uwekezaji! Wanaubariki wizi wa dhahabu! Wanaubariki wizi wa mali za umma! Wanaubariki wizi wa magogo! Wanachekelea wizi wa wanyama na pembe zao! Wanafurahia wizi wa ndege wetu wazuri! Wabunge wetu wanayaangalia yote haya lakini wamenyamaza na kuendelea kulalamika! Wasomi wetu wamekaa kimya! Wanashangilia maovu tunayotendewa (Nyangwine, 2012: 63).

Mwandishi ameonesha jinsi viongozi wa Kong'amu wanavyoubariki uwekezaji bila kuyachunguza madhara yake yanavyowaingiza wananchi katika umaskini, mateso na dhuluma.

Hali ya viongozi na wasomi kuendelea kulalamika na kutochukua hatua za kuweka misingi imara ya kuuimarisha uwekezaji kwa kuunda sera bora zinazotekelezeka kwa manufaa ya taifa, athari zake ni kubwa na ni mbaya kwa ustawi wa uchumi wa taifa. Ukosefu wa sera makini kuhusu harakati za uwekezaji pamoja na usimamizi mbaya wa rasilimali za umma umechangia kuibuka kwa migogoro mbalimbali hapa nchini kati ya wananchi, wawekezaji na serikali yao (Mayega, 2006). Kwa namna hali ilivyo sasa, viongozi hawana budi kuzipokea sera za uwekezaji kwa umakini.

Mwandishi anaonesha namna viongozi na baadhi ya wasomi wanavyorubuniwa kwa kupewa zawadi ya ufadhili na kupewa vyeo. Nyagichuro alipewa cheo cha Mkurugenzi wa Heshima wa Ubinafsishaji wa Taifa. Hali hiyo huwafanya viongozi wa Kiafrika kukosa uzalendo wa kulinda, kutunza na kubinafsisha rasilimali za umma kwa maslahi mapana ya taifa. Nyagichuro alilibinafsisha bonde la Remerera bila kutoa fidia na kuandaa eneo mbadala watakalohamia wananchi. Hali ya kutowapa wananchi eneo mbadala na fidia huwatumbukiza katika umaskini uliopindukia, mateso na hali ngumu ya maisha.

Viongozi wa Kiafrika wamechorwa kwa dhihaka ya kuchukulia mambo ya msingi kwa nguvu nyepesi na kushupalia mambo yasiyo na tija kwa nguvu kubwa. Hata hivyo, mwandishi anasisitiza kuwa jamii haina budi kufuata na kuchukua hatua za matukio ya kiwakati yanayopaswa kutuongoza katika maamuzi bora kwa maendeleo ya nchi. Wajibu wa viongozi katika taifa lolote ni kuziba mianya yote kwa kubuni mbinu mpya na sahihi za kuzuia kujilimbikizia mali pamoja na kuzitathimini sera za utandawazi ili kujenga uwezo wa ndani wa kujitegemea wa nchi inayohusika.

**Kuharibika kwa Misingi ya Amani na Utamaduni**

Mojawapo ya majukumu ya ubeberu ni kuvuruga misingi ya utulivu, mila na desturi za jamii katika taifa linalohusika. Mabepari huchochea vita na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe katika mataifa yanayoendelea ili wapate rasilimali za nchi hizo pamoja na kuuza silaha zao walizozitengeneza (Mohamed, 2001). Mara zote hutumia neno jepesi la kuleta demokrasia huku wakitumia mwanya huo kujinufaisha. Tumeshuhudia mapigano ya ndani katika mataifa mbalimbali ya Kiafrika na kwingineko ulimwenguni yanayochochewa na mabeberu. Mwandishi anaeleza:

> Kwani hao wanafanya shughuli gani? Wanasafirisha zana za vita kwenda kuuza. Sijui, lakini nasikia kuna familia kadha zinagombana na hawa wanaamini karibuni watapigana, wanataka kuwahi soko hilo (Wamitila, 2002: 146).

Jambo hili linaonesha kuwa mapigano yanayoripotiwa mahali pengi duniani, baadhi yake yanachochewa na mabeberu kwa madhumuni ya kuuza bidhaa zao za kivita. Kwa mfano, inawezekana lengo la vita visivyokwisha katika mataifa kama vile Kongo, Somalia na Sudan Kusini ni lile lile la mabeberu. Zaidi, leo tunashuhudia machafuko ya hapa na pale, nchini Libya, Yemen na Syria. Msimamizi wa masuala yote haya ni taifa la Marekani. Matokea yake, hali ya usalama imevurugwa na uchumi kuporomoka katika mataifa hayo.

Kuhusu kuenzi asili, Mihanjo (2010) anasisitiza kuwa hakuna ustaarabu wowote duniani ambao kufikia sasa umejengwa juu ya misingi ya kuiga ustarabu wa watu wengine. Kwa kawaida, desturi huanza kama tabia ya mtu au ya kundi na baadaye ikizoeleka huwa ndiyo namna halali ya mtu au watu kutenda. Kadiri muda unavyopita, ndivyo mazingira ya jamii hubadilika huku baadhi ya mila na desturi zikionekana kupitwa na wakati. Mabadiliko hayo huifanya jamii kubuni mila na desturi zinazokwenda na wakati kulingana na mahitaji ya jamii.

Nguzo za utamaduni ni mila, desturi, lugha, michezo na historia yake. Utamaduni ndicho kitambulisho kikuu cha taifa lolote; na ni kielelezo cha utashi na uhai wa watu wake. Mila na desturi ndizo huhalalisha matendo ya jamii. Jambo la kusikitisha ni kwamba, utamaduni wa Mwafrika unaendelea kudhoofishwa kwa kutumia propaganda za Kimagharibi za kueneza utamaduni wao. Vijana wa Kitanzania wanatazamishwa mambo ya Kimagharibi ili wasahau utamaduni wao (Simeon, 1997). Matokeo yake, hukosa mwelekeo wa nini cha kushika na kufuata. Kuhusu jambo hili, mwandishi wa riwaya ya *Bina-Adamu* anaeleza:

> Hawa wanangojea kuangalia filamu za *Star Wars*, *Rocky V* na *Missing Action*. Filamu za huku kwetu hawazitazami tena. Hizi video na filamu ni propaganda isiyokuwa ya moja kwa moja. Zinatumiwa kusambaza na kutangaza taswira maalumu za utamaduni mmoja tu. Ni ubeberu huu (Wamitila, 2002: 40).

Uthibitisho wa jambo hili ni kutapakaa kwa *CD*, *VCD*, *DVD* na kaseti za redio zilizojaa maonesho ya mambo, nyimbo na mitindo ya Ulaya na Marekani ambavyo vijana wengi wanavifahamu vizuri zaidi hata kuliko mambo yaliyopo katika jamii zao hapa nchini. Pia, mwandishi ametumia visakale kuonesha jinsi jamii za dunia ya tatu zinavyopuuza mambo ya ndani na kuiga ya kigeni. Baadhi ya wahusika

aliowatumia mwandishi kufafanua jambo hili ni Mwanaume, Mwanamke, Babu na Nyanya kama anavyoeleza:

> Maisha yetu yangekuwa mazuri lakini yana ukiwa wa ajabu; uhusiano kati ya watu ulikufa zamani; wakasema kuwa tulifanya kosa fulani huko nyuma. Mwanaume alimkatiza na kumalizia, 'Ehh kuna mkoba fulani tulioambiwa ulipotezwa jana yamkini ungepatikana maisha yetu yangekuwa afadhali (Wamitila, 2002:119).

Kisa hiki ni simulizi ya kale kuhusu jinsi Waafrika wanavyoacha utamaduni wao na kuiga mambo ya nje ambayo kwa hakika hayana tija kwa muktadha wa Tanzania na Afrika kwa jumla. Hali ya kupuuza mila na desturi zetu za Kiafrika, matokeo yake ni kupata taifa la watu wasiojitambua, wasio na udadisi na wasioweza kuthubutu. Jambo hilo ni hatari kwa taifa kwa kuwa ni mojawapo ya utumwa wa kiutamaduni. Ibsen (1982) anafafanua dhima ya kujenga misingi imara ya utamaduni wa taifa. Anasisitiza kuwa taifa lililo hai ni lile lenye kujenga misingi bora ya utamaduni wa jamii yake. Fani za utamaduni ni nguzo kuu ya kujengea utamaduni wa jamii na taifa lolote. Utamaduni hujengwa na mila na desturi za jamii kama vile jando, tambiko, unyago na nyimbo za kijamii. Anaongeza kuwa fasihi ina uwezo wa kujenga utamaduni wa taifa. Kwa hiyo, ipo haja ya kujenga misingi bora na imara ya utamaduni wa taifa.

Suala la kuhifadhi utamaduni wa taifa linapaswa kuchukuliwa hatua mahususi zitakazohakikisha unahifadhiwa na kuendelezwa kwa manufaa mapana ya taifa. Utamaduni wa Waafrika umekuwa ukipotea siku hadi siku kutokana na umri wao, magonjwa au kusahau baadhi ya mambo kabla ya kuenezwa vyema katika jamii zao (Searle, 2010). Jamii za Tanzania zina historia ya muda mrefu ya kukabiliwa na tatizo la kupotelewa na mambo yao ya jadi. Hali hii inatokana na kutokuwa makini katika matumizi ya njia bora za kuhifadhi na kuyaendeleza masuala ya kiutamaduni hapa nchini.

**Kigugumizi cha Kufanya Mabadiliko ya Sera**

Kwa namna hali ilivyo sasa, miundo ya siasa, utamaduni na uchumi wa dunia inabadilika kwa kasi kutokana na mwingiliano mkubwa wa jamii za kimataifa. Hali hii imetokana na mabadiliko makubwa ya mifumo ya kiuchumi ya ulimwengu. Kwa sasa, si jambo la kushangaza kuona kwamba utaratibu uliokuwa wa kawaida hapo kabla unaelekea kufikia ukomo wake (Farnandez, 1971). Mahali pake taratibu panaanza kuchukuliwa na kile kinachoitwa mikataba ya kimataifa ambayo inavuka mipaka ya taifa na kuunganisha dola na dola katika sekta zote za mataifa ya ulimwengu. Mambo hayo yameletwa na mfumo wa kibepari ambao una athari kubwa katika maendeleo ya nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania.

Athari za ubepari kupitia utandawazi haziishii tu katika uwekezaji, bali huenda mbali zaidi hadi kwenye uporaji wa rasilimali za wananchi wazawa na taifa kwa ujumla wake. Kwa sasa, malalamiko yanasikika kila mahali. Watu wanaondolewa kwa nguvu katika maeneo yao ya kuishi kwa kisingizio cha kupisha uwekezaji. Wazawa wanafukuzwa katika ardhi yao kwa kutumia vyombo vya dola vya nchi bila fidia, taarifa wala majadiliano (Mpangala, 2007). Tanzania haiwezi kuukwepa mfumo huu, isipokuwa kwa kuurekebisha kwa kuunda kanuni na sheria zinazozingatia maslahi ya taifa na sera za uwekezaji za kimataifa. Jambo hili tayari limeshawajeruhi wananchi wengi kwa namna mbalimbali. Katika riwaya ya *Msomi Aliyebinafsishwa*, jambo hili linasawiriwa pale Nyagichuro anapozuru Kong'amu huku wananchi wakiwa tayari wamejeruhiwa na ubinafsishaji. Mwandishi anaeleza:

> Zoezi letu la ubinafsishaji limetuletea maendeleo na ustaarabu mkubwa sana. Sera yetu ni kubinafsisha kila kitu! Hivyo, nawaombeni muunge mkono kwa dhati sera hii ambayo kwa sasa ndiyo dira ya taifa letu. Zidumu fikra sahihi za uwekezaji na ubinafsishaji. Wawekezaji wetu wametuletea nuru hapa nchini na kwenye bara letu zima la giza! Ubinafsishaji umetuwezesha kuwa na sera ya taifa! Nayo ni sera ya kujitegemea. Ubinafsishaji ni mzuri (Nyangwine, 2012:72).

Hotuba hii iliendelea kuvunja matumaini ya wananchi kuhusu hatima ya madhara ya uwekezaji katika jamii yao. Ubinafsishaji ulisababisha ufukara wa kutupwa kwa wananchi katika vipindi vyote vya historia yao. Watetezi wa rasilimali za nchi wanashauri kuwekeza kwa kufuata miongozo ya taifa, lakini hawasikilizwi (Chachage, 2002). Wananchi wanashuhudia jinsi rasilimali za taifa lao zinavyoporwa na kuvunwa kwa kasi bila kuwanufaisha. Jambo hili halina budi kufanyiwa mabadiliko makubwa ya kimkakati ili sera za uwekezaji ziimarike kwa kuzingatia maslahi ya wananchi na taifa katika muktadha wa mazingira ya Kiafrika.

**Hitimisho**

Kutamalaki kwa utandawazi katika jamii za Kiafrika kumesababisha matatizo makubwa yanayozigharimu nchi zinazohusika. Waandishi wa riwaya teule wamefaulu kwa kiasi kikubwa kueleza hali halisi iliyoakisiwa katika jamii zilizolengwa. Viongozi hawana budi kujitathmini, kujikosoa na kusahihisha sera za uwekezaji ili zisawiri hali halisi ya mazingira yao, uchumi wao na siasa zao kulingana na hatua za maendeleo yao. Nchi za Kiafrika hazina budi kuchukua hatua imara za kufanya marekebisho ili sera za utandawazi ziwe na manufaa. Bila kufanya hivyo, matatizo yaliyodokezwa katika makala hii yataendelea kuathiri na kudhoofisha kila fani ya maendeleo.

**Marejeleo**


Amatubi, M. (2002). 'Globalization and Mainstreaming of Kiswahili Research in the 21St Centuary' Katika *Utafiti wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Maseno, uk. 43-48.

Bhalla, A. (2006). *Globalization, Growth and Marginalization*. Canada: IDRC.

Chachage, S. C. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam: E & D Company.

Farnandez, J. (1971). *Persuasions and Performances of the Beast in Everybody and the Metaphor of Everyman: Myth, Symbol and Culture*. New York: Norton and Company.

Ibsen, J. H. (1982). *An Enemy of the People*. Denmark: Copenhagen Publishers.

Hussein, E. (1971). *Wakati Ukuta*. Nairobi: East Africa Publishing House.

Kamau, S. N. (2005). *Kiswahili, Utandawazi na Umoja wa Afrika.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Krantz, L. (2001). *The Sustainable Livelihood Approach to Poverty Reduction: An Introduction*. New York: Oxford University Press.

Jauch, H. (2001). *Playing the Globalisation Game: The Implications of Economic Liberalisation for Namibia.* Windhoek: Labour Resource and Research Institute (LaRRI).

Kivutha, K. (1999). *Kanzala*. Nairobi: Claripress.

Little, D. (1996). 'Grobalization and Education Research: Whose Context Counts?' *International Journal of Development*. Vol. 16, No. 4. pp. 427-438.

Mayega, P. (2006). *Mwalimu Mkuu wa Watu*. Dar es Salaam: MBP Interprises.

Mbise, I. (1996). *Creative Writing*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbonde, J. (2005). 'Methali za Kitandawazi'. Katika *Makala ya Kongamano la Jubilee ya Miaka 75* ya TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mihanjo, A. (2010). *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa*. Morogoro: Turiani.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Publiation Ltd.

Mpangala, G. P. (2007). 'The Role of Civic Soiety in the 2005 General Election in Tanzania', In *Tanzania Journal of Development Studies*, Vol 7, No. 2: pp. 1-18.

Murray, A. (2000). *Public Sector Restructuring in Namibia – Commercialisation, Privatisation and Outsourcing: Implication for Organised Labour*. Windhoek: LaRRI.

Mwalongo, W. (2015). 'Viashiria vya Udikteta Vinaiua Afrika'. www.mwanahalisionline.com

Nicol, B. (2002). *Postmodernism and the Contemporary Novel: A Reader.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Nyangwine, N. (2012). *Msomi Aliyebinafsishwa*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers. Vol.16, No.4. uk. 427-438.

Offiong, D. (2001). *Globalisation: Post-Neodependency and Poverty in A frica*. Enugu Nigeria: Fourth Dimension Publishing Co.

Ryanga, S. (2002). 'The African Union in the Wake of Globalization: The Forgetten Language Dimension'. Katika *Kiswahili* Juzuu 65. Dar es Salaam: TUKI. uk. 1-15.

Searle, J. (2010). *Making the Social World: The Structure of Human Civilization.* USA: Oxford University Press.

Selden, R. (1990). *The Theory of Criticism*. New York: Longman.

Sengo, T. S. Y. (1973). 'Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii', katika *Jarida la Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Simeon, K. (1997). *Desturi na Mila za Wapare*. Lushoto: Vuga Press.

Sullvan, T. (1994). *Key Concepts in Communication and Cultural Studies*. Canada: Routledge Press.

Timammy, R. (1990). *Uhakiki wa Ngano za Kiswahili*. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila, K. W. (2002). *Bina-Adamu*. Nairobi: Focus Publications Limited.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.